**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**
**SHULE YA MSINGI MATONDO**
**MTIHANI WA MAJARIBIO DARASA LA NNE MWEZI JULAI -2024**

# KISWAHILI

JINA ____________________________________________

## SEHEMU A: IMLA (Alama 10)

1. Sikiliza sentensi zinazosomwa kisha ziandike kujibu swali la (i) – (v)

   i. ____________________________________________

   ii. ____________________________________________

   iii. ____________________________________________

   iv. ____________________________________________

   v. ____________________________________________

## SEHEMU B: MATUMIZI YA LUGHA (Alama 10)

2. Jibu swali (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya sahihi na kuandika katika kisanduku kilichoko pembeni mwa kila swali.

   i. Wingi wa neno "Jiko" ni ____________
   A. Majiko B. Jiko C. Mijiko D. Meko [ ]

   ii. Amina alifika kwa ______________ kwa lengo la kusuka nywele.
   A. Msukaji B. Msusi C. Msukwaji D. Msuzi [ ]

   iii. Koti fupi lisilo na mikono huitwa?
   A. Joho B. Surupwenye C. Kizibao D. Kikoi [ ]

   iv. Kiambishi "na" hutumika kuonesha tendo linalotendeka __________
   A. Wakati uliopo B. Wakati uliopita C. Wakati ujao D. Hali ya mazoea [ ]

   v. Zao linalotokana na chikichi huitwaje?
   A. Mchaichai B. Mawese C. Tende D. Nazi [ ]

## SEHEMU C: METHALI, NAHAU NA VITENDAWILI (Alama 10)

3. Kamilisha methali,nahau na kutegua vitendawili,.

   i. Nini maana ya kitendawili "tajiri wa rangi" __________________________

   ii. Kamilisha methali isemayo "**mvumilivu** ________________________________

iii. Nini maana ya nahau "amepata jiko"? ______________________________________

iv. Malizia methali hii **"Pole pole ndio "** ni ________________________
____________________________

v. **"Amevaa miwani"** ni nahau yenye maana ya __________________________________

**SEHEMU D: UTUNGAJI (Alama 10)**

4. Pangilia sentensi zifuatazo kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E ili ziwe katika mpangilio wenye mantiki.

i. Alipotazama upande mwingine akaona nyanya zimezagaa chini pembezoni mwa barabara [ ]

ii. Alipoangalia katikati ya barabara aliona mtu amelala chini. [ ]

iii. Siku ya Jumatano Bahati aliamka mapema na Kwenda shuleni. [ ]

iv. Akamsogelea yule mtu na kisha kumsogeza kandokando ya barabara. [ ]

v. Njiani alikuta ajali ya mtu ameanguka na baiskeli. [ ]

SEHEMU E: UFAHAMU (Alama 10)

5. Soma Habari ifuatayo kwa makini kisha jibu swali (i) – (v)

Katika Kijiji cha Makongati aliishi mfanyabiashara aliyeitwa Chakubanga. Chakubanga alikuwa akimtumia mnyama jamii ya punda katika sshughuli zake za biashara. Siku moja aliamka asubuhi kisha akajiandaa yeye na punda wake tayari kwa safari ya Kwenda sokoni. Alipakia magunia manne ya chumvi kwa kuwa ilihitajika sokoni. Wakiwa safarini mfanyabiashara alihitaji kukatiza katikati ya mto ili wavuke ng'ambo ya pili yeye na punda wake. Chakubanga na punda wake walipofika katikati ya mto punda aliteleza akaanguka katikati ya maji, punda alijihisi faraja kwa kuwa hakuwa na mzigo baada ya chumvi kuyeyuka katikati ya maji. Mfanyabiashara alihuzunika sana akarudi nyumbani akampatia punda wake chakula, punda alifurahi sana.

Siku iliyofuaata mfanyabiahara aliamua kupeleka pamba sokoni, walipofika eneo lilelile la kuvuka mto, punda alijiangusha tena kwa lengo la kupunguza mzigo kama ilivyokuwa kwa chumvi. Looh!! Punda alipoamka mzigo ulikuwa mzito mara dufu, punda hakujua kuwa pamba hufyonza maji, punda alijilaumu kwa kufanya kitendo kile. Tangu siku hiyo punda hakujiangusha katika maji akiwa na mzigo kwa lengo la kupumzika na kupewa chakula.

i. Chakubanga aliishi katika Kijiji kinachoitwa? ________________________________

ii. Punda alijihisi nini baada ya kuanguka katikati ya maji akiwa na magunia ya chumvi?
_______________________________________________________________

iii. Kwanini pamba ilikuwa nzito baada ya punda kujiangusha katika maji?
_______________________________________________________________

iv. Je, Chakubanga alihisi nini baada ya chumvi kuyeyuka katika maji?
_______________________________________________________________

v. Ni kwa nini Chakubanga alihuzunika sana pale punda alipoanguka katikati ya maji?
Kwasababu__________________________________________________

**KISWAHILI – MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**

| SWALI | JIBU |
|---|---|
| 1. | i. Fikiri kabla ya kutenda<br>ii. Bilinganya hustawi sana bustanini<br>iii. Mvua za masika zimekaribia<br>iv. Loo! Amelala bila kula<br>v. Tii sheria bila shuruti |
| 2. | i. D<br>ii. B<br>iii. C<br>iv. A<br>v. B |
| 3. | i. Kumenya ndizi mbivu<br>ii. Hapotei njia<br>iii. Fedha kidogo<br>iv. Haraka haraka haina baraka<br>v. Amelewa pombe |
| 4. | i. E<br>ii. C<br>iii. A<br>iv. D<br>v. B |
| 5. | i. Makongati<br>ii. Alihisi Faraja<br>iii. Pamba hufyonza maji<br>iv. Alihisi huzuni<br>v. Alipata hasara chumvi kuyeyuka |

## IMLA

i. Fikiri kabla ya kutenda
ii. Bilinganya hustawi sana bustanini
iii. Mvua za masika zimekaribia
iv. Loo! Amelala bila kula
v. Tii sheria bila shuruti

## IMLA

vi. Fikiri kabla ya kutenda
vii. Bilinganya hustawi sana bustanini
viii. Mvua za masika zimekaribia
ix. Loo! Amelala bila kula
x. Tii sheria bila shuruti

## IMLA

xi. Fikiri kabla ya kutenda
xii. Bilinganya hustawi sana bustanini
xiii. Mvua za masika zimekaribia
xiv. Loo! Amelala bila kula
xv. Tii sheria bila shuruti